# “ Ulemavu barani Afrika ”

## EPISODE 1: " Hakuna mkamilifu "

**AUTHOR**: **Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo**

**List of characters / Episode one:**

**Msimulizi**

**<u>SCENE ONE: OLUANDA AND HIS THREE FRIENDS AFTER SCHOOL</u>**

- Oluanda (mume,18)
- Karemi (mume,18)
- Magoto (mume,18)
- Chitoto (mume,19)
- Tofa (mke, 40)

**<u>SCENE TWO: AT KAREMI’S HOMESTEAD</u>**

- Karemi (mume,18)
- Zabibu (mke, 15)
- Theresa (mke, 65)

**<u>SCENE THREE: AT THE GREAT BAOBAB TREE</u>**

- Chitoto (mume, 19)
- Oluanda (mume, 18)

**<u>SCENE FOUR: NIGHT AT CHITOTO’S HOMESTEAD</u>**

- Fagilio (mume, 42)
- Tofa (mke, 40 )
- Chitoto (mume, 19)

**UTANGULIZI:**

Salamu furifuri na karibuni tena katika kipindi cha **Noa bongo, jenga maisha yako**. Kaa nasi, kwa vipindi kumi vya kuigiza redioni, tukiangazia " **Walemavu barani Afrika** ". Jamii isiyosikika wala kupewa kipa umbele.Kupitia tamthilia hii redioni tungependa kuyaweka peupe masaibu ya watu hawa wasio thaminiwa. Tunalifungua jamvi la riwaya hii Maganye, sehemu kame na yenye dhiki. Hakuna la muhimu kupahusu,isipokuwa hutambulika kwa tamasha moja kubwa mwakani: mashindano ya upelekaji magari ambayo hupitia humo. Isipokua mwaka huo, tamasha hiyo, ingeliyageuza maisha ya kijana mmoja, kwa jina, Oluanda. Tunapiga bismillahi ambapo Oluanda na ahli zake watatu, Karemi, Chitoto na Magoto wanapanga jinsi watakavyokwenda kuyatazama mashindano hayo. Endelea kusikiliza makala yetu katika kipindi cha kwanza kwa isimu " **Hakuna mkamilifu**"

**SCENE ONE: OLUANDA AND HIS THREE FRIENDS AFTER SCHOOL**

1. **SFX: Outside ambience, birds, cars from a distance**

2. **HUGE LAUGHTER FROM THE FOUR BOYS – four boys laughing heartily)**

3. **CHITOTO**: Karemi, unanichekesha! siamini Eh? Oluanda na Magoto, yaani Karemi hawajawahi kutongoza msichana yeyote. (**laughs out even louder)**

4. **MAGOTO:** (**surprised)** Hapana! Basi itatubidi tumtafutie msichana.

**5. OLUANDA:** Mimi simo. Mamangu akijua nimehusika kumtafutia Karemi msichana, ataukata urafiki wetu.

6. **CHITOTO:** **(still laughing**) Nyinyi ni rafiki wa vipi? Mmoja ni "softiii", mwengine, mtoto wa mama… nimeanza kujishuku sina marafiki wa kisawasawa…

7. **KAREMI:** Chitoto, usiniite "softiii"! (**annoyed)**

8. **OLUANDA:** Na mimi si mtoto wa mama!

9. **CHITOTO:** Sawa basi, nihakikishieni, kwa vitendo sio maneno. Leo usiku, mashindano ya magari yatapitia Maganye. Sijawahi kuyakosa tangu nilipokuwa miaka sita. Na ili kuona vizuri, huwa napanda juu ya ule mbuyu mkubwa. Kama munamaanisha yale

munayosema, basi tukutane chini ya ule mbuyu mkubwa saa mbili usiku. Kosa uchekwe!

.

10. **MSIMULIZI:** Lakini.. kukubali ushawishi wa rika mwenzio kutasababisha nini? Oluanda na Karemi walikubali mpango wa Chitoto na ili kutimiza hayo walihitajika kutoroka makwao ili kushuhudia mashindano hayo ya magari yaendayo kwa kasi na kuacha vumbi jingi nyuma, kisha yenye hatari. Baadaye,siku hiyo jioni nyumbani kwa kina Oluanda..

**11. SFX: EVENING AMBIENCE AND POULTRY SOUNDS**

12. **TOFA:** Oluanda! Oluanda! Mbona kuku hawajaingizwa bandani?

13. **OLUANDA:** Pole mama, nilisahau. Acha niwaingize..

14. **TOFA:** Umesahau!? Yani kuku unasahau kuwaregesha bandani lakini mayai asubuhi huwa husahau kuyala. **(angry voice)** Mmh... ni juzi tu umefikisha miaka kumi na nane, tayari mambo madogomadogo umeanza kuyasahau. Haya itakuaje ukitimia miaka 60, 70 au 80? Ela utakumbuka jina lako?

15. **OLUANDA:** Nisamehe nawe mama. Kweli nimekumbuka kitu!

16. **TOFA:** Ajabu. (**sarcastic)** Haya.. ni nini?

**17. SFX : DOOR BOLT OPENED AND THEN LOCKED WITH POULTRY BACKGROUND NOISES**

18. **OLUANDA:** Nilisahau daftari langu la somo la historia kwa Chitoto. Aliniazima kunukuu somo hilo leo darasani. Niende kwao haraka nikakichukuwe? Sitakawia.

19. **TOFA:** Ni mara ngapi nimekukanya na yule kijana? Hana heshima, mtundu na mtovu wa adabu! Wazazi wote hapa Maganye hawampendi. Isipokuwa babake, Fagilio. sawa, natema mate ardhini na … Kabla…

20. **OLUANDA:** Kabla yakauke niwe nisharudi.Mama umenieleza hayo tangu niko na miaka mitano.. Nafahamu vyema kabisa... (**off mic**) Sikawii….

21. **<u>MSIMULIZI:</u>** Alipomuongopa Tofa, mama yake kwa mara yake ya kwanza, Oluanda aliipa kisogo nyumba yao na kuisalimu anga iliyotanda kiza ya Maganye. Alipapita haraka nyumbani kwa kina Karemi, kwa kina Magoto, na akasimama kidogo kwa kina Kangwa. Kangwa alikua binti mrembo pale Maganye,ambaye alimvutia kila mvulana kumuoa. Lakini Oluanda alijuwa hilo halingewezekana. Mwisho, aliuona mbuyu mkubwa ambao matawi yake yalifunuka kama viganja vinasubiri kupokea kitu . Na kwa umbali, aliliona umbo la Chitoto. Lakini kwanza, hebu tuingie katika makao ya kina Karemi, na tumjue dadake Zabibu na nyanya yao Theresa.

**<u>SCENE TWO: AT KAREMI’S HOMESTEAD</u>**

**22. SFX: FIRE BURNING IN FIREPLACE**

23. **ZABIBU:** Nyanya, nahisi njaa.. uji utaiva saa ngapi?

24. **THERESA:** Hivi unatokota. Lakini kaa kando na jiko au moto. Utakuchoma na kukuharibu macho. Kaa huko kizani. Huko ndio watu weupe na wenye macho ya samawati wanakokaa. La sivyo...

25. **KAREMI:** La sivyo nini ? Nyanya, Zabibu ni zeruzeru, wala si popo wakukaa kizani! Mbona huwa hautaki atoke nje? Lau wazazi wangu wangelikuwako hai sidhani kama wangelikubali haya!

26. **THERESA:** (**Bitter voice**) Lakini hawako! Sasa utanisikiza mimi.. wewe bado umdogo sana, umenisikia?

27. **ZABIBU:** (**Sadly**) Mbona niko hivi, mbona nikazaliwa hivi, mbona wazazi wangu wakafa na kutuacha hivi?

28. **THERESA:** (**Comforting her)** Nyamaza mwanangu, usilie. Nyanya Theresa hatakuacha. Rudi ukakae kibaoni kwako , nakuletea uji unywe. (**to Karemi)** Ushafurahi sasa, Karemi. Huoni aibu wewe.

**29. SFX : PORRIDGE BEING POURED INTO BOWLS**

**30. Msimulizi:** Hapo ndipo pahala Karemi and Zabibu, aliyezaliwa na hitilafu ya rangi ngozini, zeruzeru, wanaishi. Mayatima wawili, waliopoteza wazazi wao katika ajali ya barabarani, waliachwa kulelewa na ajuza nyanya yao, Theresa. Naam, sasa tuelekee katika ule mbuyu mkubwa

**SCENE THREE: AT THE GREAT BAOBAB TREE**

**31. SFX: : CHIRPING OF BIRDS, CRICKETS etc. (SAME UNIQUE WHISTLE HEARD FROM OLUANDA)**

32. **CHITOTO:** (**commanding voice** ) Kimya! Wewe unatoka wapi, Oluanda? Kwani hujui kupiga mbinja usiku haswa mibuyuni huleta nuksi?

33. **OLUANDA:** Samahani , nili… nilikuwa nimesahau Karemi?

34. **CHITOTO:** Yule 'softii' kama kawaida yake haji. Sishangai lakini mtu ambae hawezi kutongoza msichana, hawezi kufanya yale tutakayofanya, muache akae nyumbani na dadake mwenye 'ngozi yakuazima".

35. **OLUANDA:** ''Ngozi yakuazima''? Chitoto, Zabibu hana ngozi yakuazima, Zabibu amekosa "melanini"mwilini, ambayo hufanya ngozi yetu nyeusi, tulifunzwa hivyo shuleni. Sasa magari yatapita saa ngapi?

36. **CHITOTO:** Hivi punde. Uko tayari? Sawa, nitakushikia mwenge uweze kuona tukiwa hapa.utahitajika kupanda juu zaidi, nakwambia, hutaamini….

37. **OLUANDA:** Hmm, na huku ni kweusi mno, giza limetanda, kunatisha. Unahakika umekuwa ukija huku kwa miaka mingapi? Miaka nane?

38. **CHITOTO:** Sasa mtoto wa mama! Utaparaga au? Mimi sitaki kupitwa na maonyesho.

39. **OLUANDA:** Sawa. Twende kazi basi. Niwashie mwenge.

**40. SFX: TORCH SWITCHED ON, OLUANDA ACTS OUT CLIMBING A TREE, rustling of branches and leaves**

41. **CHITOTO:** (**in a loud voice**) Juu! Panda juu zaidi Oluanda!

**42. SFX : : BREAKING OF BRANCH FOLLOWED BY BODY THUMPING ON GROUND**

43. OLUANDA: (**in excessive pain**) Arrrrrgh!..mguu wangu!..Arrrrrgh! Chitotoooooo. nisaidieeeee.

44. CHITOTO: La hapana! Wewe una nuksi. Si nilikwambia usipige mbinja usiku. Shauri yako. Pole Oluanda lakini sikuwa na wewe.

**45. SFX: FOOSTEPS RUNNING AND FADING AWAY, rally car noise from a distance, coming closer an closer, passing by**

46. **OLUANDA** : **(Crying out**) Laaa! Chitoto tafadhali njoo! Mamaaaaa!.. nisaidiee!..( **In great fear)** Oh hapana, magari yanakuja! Nisipoondoka njiani… Uurgh..uurgh(**acts out crawling on ground)** Tafadhali…Simama.. hapana!…

**47. MSIMULIZI:**

Oluanda alimpigia usiyaa dereva asimame lakini sauti yake ilifunikwa na kelele za magari yaliyopita kwa kasi. Yule dereva, ambaye hakumuona Oluanda, alimvyoga mguu wake wa kushoto, akausaga tikitiki, na akaacha nyuma vumbi lililomtifukia Oluanda akilia kwa uchungu. Oluanda alizidiwa na maumivu na kupoteza fahamu na kuzimia. Je kutatokea nini sasa? Tofa, mamake Oluanda, aliingiwa na wasiwasi alipotambua mwanawe kakawia sana kwa kina Chitoto, na kama ada ya mzazi yeyote akafulizia nyumbani kwa kina Chitoto na kupokewa na Fagilio, babake chitoto aliyekua mlevi chakari.

<u>**SCENE FOUR: NIGHT AT CHITOTO'S HOMESTEAD**</u>

**48. SFX: ambience, crickets, KNOCKING ON DOOR**

49. **FAGILIO:** (**Drunken voice**) Nani huyo? Ingia ... lakini bora uwe una gilasi ya pombe.

50. **TOFU:** La, sina pombe yeyote na sikujia hayo Fagilio. Nimekuja kumuulizia kijana wangu. Aliondoka...

51. **FAGILIO:** Kijana wako? Unamaanisha Oluanda. Hayuko hapa.

52. **TOFU:** Haiwezekani! Oluanda alitoka nyumbani kuja hapa kuchukua kitabu chake cha historia... yuwapi mwanao Chitoto?

53. **FAGILIO:** Mwanamke chunga mdomo wako ukiwa nyumbani kwangu! (**Calls out)** Chitoto! Njoo hapa!

54. **CHITOTO:** (**With guilt**) Habari… Shikamoo Mama.

55. **TOFU:** (**Cuts him short)** Chitoto, yuko wapi Oluanda? Na usinidanganye kwa sababu unajua aliko.

56. **FAGILIO:** Tofa!...usimkaripie mwanangu mbele yangu. Huyu si Oluanda.

57. **TOFU:** (**Calm but firm )** sawa , Chitoto, yuwapi Oluanda?

**HITIMISHO:**

Asijuwe la kusema na asione pakutorokea, Chitoto alisimama mbele ya Tofa, mamake Oluanda na babake Fagilio. Na hapa tunafikia hatima ya kipindi chetu cha kwanza katika masaibu ya walemavu barani Afrika. Kweli chitoto atasema ukweli? Oluanda aliumia kiasi gani? Ja, atapona? Je, Zabibu dadake Karemi ambaye ni zeruzeru, ataishi Maisha ya kawaida kama watoto wengine? Au atakuwa mtengwa wa mila na desturi? Kwa haya na mengineyo, usisahau kuwa nasi juma lijalo!

Ili kusikiliza tena kipindi hiki au chenginecho cha Noa bongo,jenga maisha yako, tembelea tovuti zetu **www.dw-world.de/lbe.**

Alamusiki. Kila la heri hadi tutakapokutana tena!